# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

## MAGHABE HIGH SCHOOL

***Motto:Kumcha Bwana Ni Chanzo Cha Maarifa***

**S.L.P 3785 MBEYA.**

***SIMU:*0754893508/0756543183/0788245325/0759000721**

**Fax: 0252504068**

***Email:***maghabe2020@gmail.com: **Website: www.maghabehighschool.ac.tz**

**MZAZI/MLEZI WA.....**
**S.L.P.....**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAGHABE HIGH SCHOOL**
**KIDATO CHA .....2021**

**(JOINING INSTRUCTIONS)**

Ninafurahi kukujulisha kwamba mtoto wako amechaguliwa kujiunga na Shule hii kidato cha……mwaka 2021. Ninakupongeza wewe Mzazi/Mlezi pamoja na mtoto.

1. **SHULE ILIPO:**

Shule ipo Mkoani Mbeya Wilaya ya Mbeya (v) katika mji mdogo wa Mbalizi eneo la Utengule, kilometa 17 kutoka Mbeya Mjini na kilometa 5 kutoka mji mdogo wa Mbalizi, barabara kuu iendayo Mkwajuni – Chunya.

Shule ni ya mchanganyiko Wavulana na Wasichana.

**2.MASOMO YANAYOFUNDISHWA:**

1. BASIC MATHEMATICS (HISABATI)
2. CIVICS (URAIA)
3. KISWAHILI
4. ENGLISH (KIINGEREZA)
5. HISTORY (HISTORIA)
6. GEOGRAPHY (JEOGRAFIA)
7. PHYSICS (FIZIKIA)
8. CHEMISTRY (KEMIA)
9. BIOLOGY (BIOLOJIA)
10. BOOK KEEPING
11. COMMERCE

1. **MICHANGO Tshs. 260,000/=(NJE YA ADA)**ni kwa ajili ya :-

(i) T. shirt mbili
(ii) Usajili
(iii) Kitambulisho
(iv) Ukarabati

∗Fedha hii ilipwe mara moja benki pamoja na awamu ya kwanza ya ada.
* Pia aje na bima ya afya au Tsh 54.500/= hii ni kwa kila mwaka .

2. **ADA NA HOSTELI**

Gharama za hosteli pamoja na ada kwa mwaka 2021 ni Tsh**. 1,700,000/=** (millioni moja na laki saba tu.) utaratibu wa kulipa ni kama ifuatavyo;

| MWEZI | KIASI CHA KULIPA | MAELEKEZO |
|---|---|---|
| Awamu ya kwanza (Desemba) | 425,000/= | Shule inapofunguliwa |
| Awamu ya pili (Machi/April) | 425,000/= | Anapotoka likizo fupi/mid term |
| Awamu ya tatu (Julai) | 425,000/= | Anapotoka likizo ndefu |
| Awamu ya nne (Septemba) | 425,000/= | Anapotoka likizo fupi |

- Pia aje na bima ya afya au tsh 54,500/= matibabu hii ni kwa kila mwaka

**MUHIMU:**

(i) Fedha zote (Michango, Ada pamoja na hosteli ) zilipwe benki kupitia mojawapo ya Akaunti zifuatazo:-

- ***MAGHABE SECONDARY SCHOOL - NBC A/C NO. 016103005503***
- ***MAGHABESECONDARY SCHOOL – NMB A/C NO. 62506600016***

∗Ada ikilipwa hairudishwi, usilipe ada chini ya kiwango kwa awamu husika.

(ii) Malipo yakifanyika mkabidhi mtoto pay-in-slip ikiwa na jina lake ili kuepuka usumbufu usio wa lazima kwa mtoto.

- Hatupokei cheki wala cash
- Hakikisha unaleta fomu hii siku ya kuripoti

(iii) Ni lazima mtoto awe na mlezi atakayetambuliwa na shule (kwa wale watokao nje ya mkoa wa mbeya).

❖ **TAFADHARI ANDIKA JINA LA MWANAFUNZI ANAYELIPIWA ADA KWENYE BANK PAY- IN-SLIP WAKATI WA KULIPA** (USIANDIKE JINA LA MZAZI AU LA MLIPAJI)

3. **SARE ZA SHULE**

**A: WAVULANA**

- Suruali 2 nyeusi za darasani na mkanda mweusi usio na pambo lolote au picha yoyote n.k. (aje nazo shuleni akiwa amevaa) mshono malinda mawili na turn up isiwe chupa mguuni. (modo) zinapatikana shuleni kwa Tsh 20,000/= kila moja.
- Suruali 2 rangi ya kaki ambazo ni za kushindia shuleni. Mshono malinda mawili na turn up. Pia isiwe chupa mguuni (modo) zinapatikana shuleni Tsh.20,000/= kila moja
- Shati 2 rangi nyeupe mikon mifupi. (Tetron ) zinapatikana shuleni Tsh. 10,000/= kila moja

- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba (kisigino kifupi) na isiwe raba
- Soksi jozi 4 rangi nyeusi (ndefu za kawaida)zinapatikana shuleni tsh 1000/= kwa kila pair moja
- Sweta moja (01) (rangi ya damu ya mzee) zinapatikana shuleni kwa tsh 12000/=

**B: WASICHANA.**

- Sketi 2 ndefu rangi ya Orange mshono Linda box mbele moja na nyuma moja na malinda madogo matatu pembeni), zinapatikana shuleni kwa bei Tsh. 20,000 kwa kila moja
- Sketi nyeusi 2 ndefu zenye marinda ambazo ni za kushindia shuleni (linda box)zinapatikana shuleni kwa Tsh. 20,000/= kwa kila moja
- Shati 2 nyeupe mikono mifupi. (Tetron) zinapatikana shuleni kwa Tsh. 10,000 kwa kila moja.
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kamba (kisigino kifupi) na isiwe raba
- Soksi jozi 4 rangi nyeupe (ndefu za kawaida)zinapatikana shuleni kwa tsh 1000/= kwa pair moja
- Sweta moja (01) (rangi ya damu ya mzee) zinapatikana shuleni kwa Tsh. 12,000/= kwa kila moja.

**C:VIFAA VINAVYOTAKIWA BWENINI. (Kwa wote)**

- Sabuni ya unga kilogram tano (5 kg)kwa matumizi ya usafi wa shule.(inakusanywa ofisini)
- Godoro futi 2 Neti ya mviringo, shuka 2 rangi ya blue - bahari
- Vifaa vya kuogea na kufulia:- ndoo, sabuni,taulo,mafuta ya kupakaa
- Vifaa vya michezo, viatu vya michezo, jezirangi ya bluu bahari na track suit **Dark blue** pair moja zinapatikana shuleni kwa Tsh. 25,000/=
- Tranker (box la chuma) la kutunzia vifaa vyake. Pia linapatikana shuleni kwa Tsh 35,000/= tu.
- Mopa yenye mpira na mfagio mgumu wa dukani wenye mpini (hard brooms) na Mfagio wa nje (chelewa), pamoja na mfagio laini (soft broom) kwa wavulana na brush ndogo ya kusugulia tundu la choo kwa wasichana.
- Kwanja
- Blanketi dogo
- Kandambili (Ndala) isiwe yeboyebo au makurubasi.
- Sabuni ya unga (kilo moja)1kwa matumizi ya mwanafunzi.
- Mto wa kulalia foronya rangi ya pinki
- Weka alama ya jina kwenye nguo ya mwanafunzi

4. **VIFAA VINAVYOTAKIWA DARASANI**

- Daftari kubwa 12 (counter book –quire 3) zinapatikana shuleni kwa Tsh 3,000/= kwa kila moja
- Mkoba wa kubebea daftari
- Mkebe, rula biki na penseli za kutosha (vinapatikana shuleni)
- Alete Rim tatu(3) za karatasi **A4 (paperon)** ambazo zinapatikana shuleni kwa Tsh. 11,000/= aina nyingine hazitapokelewa.
- Masomo ya jioni elfu arobaini (40,000/=) iletwe cash ofisi ya Taaluma.
- Tochi kwa ajili ya matumizi ya dharula
- Mafaili (12) kumi na mbili (yawe ya prastic spring file) kwa ajili ya kutunzia mitihani yanapatikana shuleni Tsh 2000/= kila moja.

**Nakutakia Maandalizi mema na Safari Njema.**
***Kumcha Bwana ni Chanzo cha Maarifa.***

***"KARIBUNI SANA MAGHABE SEKONDARI***
***IMEANDALIWA NA***

***.....***
***MKUU WA SHULE.***

# MAGHABE HIGH SCHOOL

## *Motto:Kumcha Bwana Ni Chanzo Cha Maarifa*

## SHERIA ZA SHULE

Sheria za shule zinamsaidia mwanafunzi kuwa na tabia nzuri na kulelewa katika maadili ya Kitanzania na kidini, aidha zinamsaidia mwanafunzi kufikia lengo la kuelimishwa katika mazingira ya shule yetu. Hivyo mwanafunzi aogope wakati wote kutenda jambo lolote baya hata kama halijatajwa katika sheria za shule.

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu walimu wote na wafanyakzi wasio walimu na mtu yoyote anayemzidi umri awapo shuleni na mahali pengine popote. Kushindwa kufanya hivyo ni kosa linaloweza ***KUMSIMAMISHA AU KUMFUKUZA SHULE.***
2. Mwanafunzi akipatikana na kosa la kufanya mapenzi, wizi, ulevi, uasherati kuoa au kuolewa, kubaka, kunajisi, kulawiti au kutoa mimba, kulala nje ya shule, kubeba au kutumia madawa ya kulevya ikiwemo bangi, kutenda kosa jingine lolote la jinai, kuingia kwenye vilabu vy pombe, baa, nyumba za kulala wageni au kumbi za starehe n.k. Adhabu yake ya makosa hayo ni ***KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA BILA MSAMAHA***
3. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na bidii katika masomo yake na kufikisha kiwango cha alama kilichowekwa na uongozi wa shule katika majaribio na mitihani ya Muhula, ambacho si chini ya wastani wa**50%** watakaoshindwa kufikisha wastani huo hawataruhusiwa kuendelea na masomo katika shule hii.
4. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kufanya na kukamilisha kazi zote anazopangiwa iwe ndani au nje ya darasa. Aidha ni marufuku kwa mwanafunzi kiongozi kujiuzulu wadhifa aliopewa kidemokrasia ngazi ya kiranja, hostel na darasa, vinginevyo atahesabiwa kuwa amegoma hivyo ***KUFUKUZWA SHULE.***
5. Mwanfunzi ni lazima aheshimu kengele ya shule, hii ni pamoja na kukimbia ili kuwahi sehemu yoyote anayotakiwa bila kuchelewa, alichelewa ataadhibiwa
6. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa viatu vyenye kisigino au soli ndefu au pana, kandambili, raba, mkanda usio mweusi, wenye bakuli kubwa au mapambo mengine kama vile kofia, hereni, mikufu, kanga, bangili, nywele ndefu, ndevu, kupaka rangi kucha au nywele, kupaka wanja, kujichubua, kunyoa kipara ni kosa. Yeyote atakayepatikana na makosa haya atarudishwa nyumbani kumwita mzazi / mlezi wake, na kunyang'anywa viyu hivyo hapo juu na hatarudishiwa.

7. Mwanafunzi anatakiwa kuishi kwa amani, heshima, utii, usikivu na upendo kwa watu wote wanaomzunguka. Hivyo hapaswi kupiga, kutukana, kudharau, kufyonya, kuanzisha au kishiriki vurugu zozote zile. Kupatikana na kosa lolote katika hayo kutasababisha mwanafunzi huyu ***KUFUKUZWA SHULE BILA MSAMAHA.***
8. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Nembo ya Taifa, Fedha, picha za Viongozi pamoja na alama zingine za Taifa. Kushindwa kuzingatia hayo kutasababisha mwanafunzi ***AFUKUZWE SHULE.***
9. Mmwanafunzi anatakiwa kuvaa sare wakati wote awapo darasani, atokapo nje ya shule, aendapo kanisani, aingiapo shuleni, kwenye maandamano, anaposafiri kuja shuleni, aendapo hospitali, na wakati wowote atakiwapo kufanya hivyo, kushindwa kufanya hivyo ni kosa linalompasa ***KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.***
10. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia, viatu vyenye visigino / soli ndefu, visivyo na kamba, kuvaa kach au pambo lolote, hereni, kutoboa masikio, mikufu, kanga , bangili, pete n.k. Aidha ni marufuku kufuga kucha, nywele ndefu, kupaka rangi kucha, au nywele, kujichubua, kunyoa kipara, kufuga ndevu n.k. yeyote atakayepatikana na hayo ***atarudishwa nyumbani kumleta mzazi / mlezi wake pamoja na onyo kali na atanyang'anywa vitu hivyo bila kurudishiwa.***
11. Kila mwanafunzi lazima aheshimu tarehe ya kufungua shule. Endapo atachelewa kufika shuleni hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ***ikiwa ni pamoja na kurudishwa nyumbani kumleta mzazi / mlezi wake.***
12. Ni lazima kila mwanafunzi kuheshimu na kutunza mazingira, majengo, samani na mali nyingine za shule. Endapo mwanafunzi atafanya uharibifu, itahesabiwa kama moja ya makosa makubwa ambayo mwanafunzi atatakiwa kurudi nyumbani hadi mzazi / mlezi atakapofidia mali husika.
13. Usafi wa mwili ni sehemu muhimu ya maisha ya mwanafunzi ni lazima mwanafunzi awe msafi wa mwili wakati wote. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kuvaa mlegezo, suruali, sketi/blauzi zinazobana au kuweka mikono mfukoni, ***adhabu yake ni adhabu kali ya ndani na kurudishwa nyumbani.***
14. Lugha inayotumika darasani na nje ya darasa ni kiingereza tu, isipokuwa wakati wa somo la Kiswahili na dini. Hii itasaidia kuleta ufanisi katika masomo ***adhabu itatolewa kwa atakayekiuka.***
15. Endapo mwanafunzi atafukuzwa shule / hostel kwa kosa lolote lile gharama alizolipa kwa ajili ya ada/hosteli hazirudishwi.
16. *N*i marufuku kupiga au kupigwa katika eneo la shule bila kibali cha Mkuu wa Shule
17. Chakula kikuu cha shule ni Ugali, Wali, Maharage, Nyama ya Ng'ombe, Dagaa, Samaki, Kande na kila chakula kinaambatana na mboda za majani. Shule haina huduma kwa wenye matatizo na vyakula hivi.

18. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu, kamera CD, DVD, pasi, mishumaa, siraha ya aina yoyote mfano: - kisu, chupa n.k. Aidha haruhusiwi kuharibu kwa makusudi mali zake na za shule, kushirikiana na waharifu au kuficha vitendo viovu vinavyofanywa na wanafunzi wenzake au mtu yeyote ndani au nje ya shule, ***MAKOSA HAYA KWA KILA KOSA ADHABU YAKE NI KUFUKUZWA SHULE BILA MSAMAHA***.

19. Mwanafunzi anatakiwa kuwa safi wakati wote,kufika katika sehemu aliyopangiwa kwa wakati unaotakiwa na kuhakikisha kuwa bweni lake, darasa lake na maeneo yote ya shule ni safi wakati wote mfano :- vyoo, jiko, ukumbi n.k. kushindwa kufanya hivyo ni kosa na ***adhabu kali itatolewa.***

20. Mwanafunzi anatakiwa kuwa kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo. Aidha mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shule mda wote wa masomo ndani na nje ya darasa (Ruhusa yoyote ya kutohudhuria darasani itatolewa na Mkuu wa Shule tu au Mwalimu atakayekuwa ameteuliwa na Mkuu wa Shule kufanya hivyo, mfano: Makamu Mkuu wa Shule, Mwandamizi Taaluma, Nidhamu n.k.) kukaidi hayo ni makosa hivyo mwanafunzi anaweza ***KUSIMAMISHWA AU. KUFUKUZWA SHULE.***

21. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria na kuheshimu maandalizi ya jioni na asubuhi (Night and Morning Preparations) kushindwa kufanya hivyo mwanafunzi ***anatakiwa akamlete mzazi / mlezi. Pamoja na kupewa adhabu ya nadani.***

22. Mwanafunzi haruhusiwi kupokea mgeni yeyote shuleni.aidha Mzazi / Mlezi haruhusiwi kuonana na mwanafunzi ikiwa ulazima utajitokeza ataruhusiwa kuonana na mwanafunzi na hatuna siku maalum ya kuja kumwona mwanafunzi ***(Visiting Day).***

23. Ni lazima mwanafunzi aripoti shule inapofunguliwa na isizidi saa 11.00 Jioni, mwanafunzi atakayechelewa hatapokelewa badala yake ***atarudishwa nyumbani kumleta mzazi / mlezi***

24. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia au kutoka dirishani, kubaki bwenini, au popote asipotakiwa akifanya hivyo ***ATAFUKUZWA SHULE BILA MSAMAHA.***

25. Nilazima mwanafunzi aoneshe nidhamu ya kiwango cha juu katika maongezi na wanafunzi wenzake, walezi wake, n.k. bila kutumia lugha ya matusi / chafu, ya mtaani, kejeli, ubishi, kuzomea, kuguna n.k. ni wajibu wake kusimama kumsalimu mwalimu / mfanyakazi asiye mwalimu au Mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita au kuingia mahali popote ikiwa ni pamoja na kumpokea ikiwa amebeba mzigo au kitu chochote, vinginevyo ***ATASIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE BILA MSAMAHA.***

26. Ni makosa mwanafunzi kugoma au kugomea adhabu au maelekezo, matatizo yote lazima yatatuliwe kwa kuzingatia kanuni na taratibu za shule hii. Aidha ni marufuku kupeleka malalamiko nje ya shule moja kwa moja badala ya kupitia ngazi husika. ***MAKOSA HAYA YATAMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI BILA MSAMAHA.***

27. Mwanafunzi hapaswi kumkimbia mwalimu au mfanyakazi yeyote pale anapoitwa ikiwa ni pamoja na kusema uongo, kusingizia pindi aulizwapo mfano : kutaja jina la uongo kufanya hivyo ni kosa kubwa. ***LITAKALOMSIMAMISHA AU KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI.***
28. Ni marufuku mwanafunzi kutembelea au kuingia nyumbani kwa walimu au wafanyakazi wasio walimu bila ruhusa maalum, pia haruhusiwi kuingia jikoni ***ISIPOKUWA KWA KIBALI MAALUM.***
29. Ni marufuku mwanafunzi kudanganya kwenye mitihani yote iwe ya ndani au nje kufanya kosa hili kutasababisha mwanafunzi ***KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA BILA MSAMAHA.***
30. Ruhusa yoyote ya kutoka nje ya shule lazima iwe kwa maandishi na itolewe na Mkuu wa Shule pia ni wajibu wa mwanafunzi kupisha mwalimu / mtu yeyote aliyemzidi umri wanapopata mahitaji au huduma, kushindwa kufanya hivyo ni kosa. ***ADHABU ITATOLEWA.***
31. Mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya atatakiwa aoneshe cheti cha tatizo lake mara anaporipoti shule au apatapo tatizo hilo cheti cha Daktari wa Hospitali ya Serikali au Hospitali inayotambulika ndicho kitakubalika kionyeshwe kwa daktari wa shule, patron, matroni na kwa mwalimu mwanadamizi nidhamu.

***<u>KUKUBALI:</u> NIMESOMA NA KUZIELEWA SHERIA ZOTE NINAKUBALIANA NAZO NA NIKO TAYARI KUZIFUATA WAKATI WOTE.***

***JINA NA SAINI YA MWANAFUNZI*** ***JINA NA SAINI YA MZAZI /MLEZI***

_____ _____

_____ _____

***……..***
***MKUU WA SHULE***

# *"KARIBUNI SANA"*
# *MAGHABE HIGH SCHOOL*